

FASIHI: MUZIKI NA FASIHI YA KISWAHILI

**MCHANGO WA MUZIKI WA KIZAZI KIPYA KATIKA UFUNDISHAJI WA USHAIRI WA
KISWAHILI KWA SHULE NA VYUO NCHINI KENYA**

Meshack Onzere Mulongo

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

onzeremulongo@yahoo.com

Ikisiri

Makala hii imetokana na utafiti uliotathmini mchango wa muziki wa kizazi kipya katika ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili kwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Kenya. Makala hii itatambua changamoto zinazokabili ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili, kuchunguza uhusiano uliopo kati ya muziki wa Kizazi Kipya na Ushairi wa Kiswahili kimuundo, kimtindo na kimaudhui. Usamplishaji wa kimaksudi ulitumika. Utafiti uliwalenga walimu na wanafunzi katika shule za upili Wilaya ya Emuhaya Kaunti ya Vihiga.